

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA KWANZA

05 NOVEMBA, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 05 NOVEMBA, 2019

I. WIMBO WA TAIFA:

II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:

III. TAARIFA YA SPIKA:

IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2020/2021.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa

Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

V. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

1. MHESHIMIWA ANNA JORAM GIDARYA (VITI MAALUM)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa muda mrefu sasa Serikali imekaa kimya kuhusu ajira kwa Vijana; kumekuwa na wimbi kubwa la Vijana mitaani wasio na ajira waliomaliza Vyuo mbalimbali takriban miaka mitatu iliyopita:-

- (a) Je, ni lini Serikali itafungua milango ya ajira kwa Vijana wa Kitanzania walioneseka kwa muda mrefu;

- (b) Je, Serikali imefanya tathmini ya kiwango cha madhara yaliyotokana na Vijana kukosa ajira;
- (c) Je, ni Vijana wangapi wameathirika na kujiingiza katika makundi mabaya kwa kukata tamaa ya kupata ajira.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

2. MHESHIMIWA HASSANI SELEMAN KAUNJE (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- (a) Je, ni lini Serikali itawadhamini Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ili waweze kupata mikopo kama ilivyo kwa Madiwani na Wabunge;
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho/mishahara Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

3. MHESHIMIWA SELEMANI SAID BUNGARA (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Kilwa Masoko kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa Watumishi, upungufu wa

dawa, upungufu wa vitanda, magodoro, mashuka, vifaa tiba, kipimo cha sukari, kipimo cha damu, uchakavu wa majengo na pia Kituo hicho hakina gari la kubebea Wagonjwa hali ambayo ni kero kubwa kwa Wagonjwa wanaohamishiwa Hospitali ya Wilaya iliyo umbali wa zaidi ya kilometra 25:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto zinazokikabili Kituo hicho cha Afya ili kuondoa adha kwa Wananchi.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

4. MHESHIMIWA ALBERT OBAMA NTABALIBA (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia Kituo cha Forodha Manyovu ili kuitisha mizigo kwenda Burundi kwa kiwango cha kutosha.

WIZARA YA MADINI:

5. MHESHIMIWA AGNESS MATHEW MARWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Wananchi wengi walibomolewa nyumba zao na Mgodi wa ACACIA uliopo Nyamongo Wilayani

Tarime na wengine hawajalipwa fidia ya maeneo yao mpaka sasa. Aidha mgodi pia umeanza kuchimba chini ya maeneo ya watu (*Underground mining*):-

Je, ni lini Mgodi wa ACACIA uliopo Nyamongo utalipa fidia Wananchi hao.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

6. MHESHIMIWA ALI HASSAN KING (JANG'OMBE)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu:-

Je, ni kwa nini Serikali imepiga marufuku uvuvi wa kuzamia kwa kutumia chupa (Gas Cylinder).



WIZARA YA KILIMO:

7. MHESHIMIWA ZAINAB MUSSA BAKAR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Yamejitokeza maradhi katika mimea ya Mipapainchini ambayo yanahatarisha kupotea kwa mimea hiyo:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuweza kudhibiti maradhi hayo;

- (b) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa juu ya maradhi hayo ili kugundua yanababishwa na nini;
- (c) Kama bado; Je, Serikali haioni kuna hatari ya kupoteza mmea huo ambao ni muhimu sana.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

8. MHESHIMIWA RHODA EDWARD KUNCHELA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoa wa Katavi ni jambo ambalo linaleta sintofahamu kwa maana ya umiliki wa eneo (Hati) na ujenzi wa Chuo ambao mpaka sasa bado hakijajengwa na kusababisha jambo hili kuleta usumbufu kwa Wanafunzi kwenda Mikoa mingine kutafuta Vuyo vya Kilimo:-

Je, Serikali ipo tayari kushughulikia sintofahamu hii ya ujenzi wa Chuo hicho cha Kilimo.

WIZARA YA MAJI:

9. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji katika Kata ya Mtwango ambao umechukua muda mrefu bila kukamilika.

10. MHESHIMIWA JAMES KINYASI MILLYA (SIMANJIRO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Kuna mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mkoa wa Kilimanjaro kuelekea Arusha Mjini, mradi huu unapitia kwenye mipaka ya Wilaya ya Simanjiro Kata za Naisinyai na Mererani:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wananchi wa Kata hizo wanapatiwa huduma hiyo inayopita kwenye maeneo yao;
- (b) Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua ujenzi wa barabara ya km14 toka KIA hadi Mererani aliwaahidi Wananchi wa Mererani na Naisinyai kwamba atawakumbuka kwenye kuondoa adha ya maji; Je, Serikali imejipangaje kutimiza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

11. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mikoa ya Kanda ya Ziwa imeathirika sana

na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu mkubwa wa mazingira:-

Je, ni lini Serikali itajenga Vyuo vya uhifadhi wa Wanyamapori na uhifadhi wa mazingira na elimu ya utalii hasa baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi za Taifa za Chato Burigi, Kigosi, Ibanda, Rumanyika, Rubondo na Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

12. MHESHIMIWA KITETO ZAWADI KOSHUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Bodi ya Utalii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kutangaza utalii wa ndani ya nchi:-

Je, Serikali inaisimamiaje Bodi hiyo ili kuhakikisha Mkoa wa Mwanza unatangazwa kama Mji wa Kitalii.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

13. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Askari wa Kituo cha Polisi katika Mji wa Makambako hawana gari la doria wala nyumba za kuishi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za kuishi Askari hao;
- (b) Je, ni lini Serikali itatoa gari la doria kwa Kituo cha Polisi Makambako.

**14. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Majanga ya moto yamekuwa yaitokea mara kwa mara hasa Viwandani, Majumbani na katika majengo ya Serikali:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi na Wananchi juu ya mbinu za kujihami na kujiokoa katika majanga ya moto;
- (b) Je, Serikali imejipangaje katika kutoa mafunzo katika maeneo ya kazi na Wananchi juu ya matumizi ya mitungi ya kuzima moto (*Fire Extinguishers*);
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukagua mitungi hiyo kama bado inafaa kwa matumizi au imeshapita muda wake wa kutumika.

VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Bill, 2019*].

VII. KAMATI YA MIPANGO:

•WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**DODOMA
05 NOVEMBA, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**